

**MAONI  
JUU YA MJADALA  
BAINA YA  
MASHEIKH WAWILI**

NA

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian,  
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s.

Mfasiri  
Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA  
TANZANIA

M A O N I  
JUU YA MJADALA  
BAINA YA MASHEIKH WAWILI  
Swahili translation of *Review bar Mubāḥathah*  
*Batālwī wa Chakrīhālwī* (Urdu)

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2008  
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:  
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania  
Mnazi mmoja, Dar es Salam.  
Simu: +255222110473  
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:  
Ahmadiyya Printing Press  
Dar es Salam. Tanzania  
Simu: +25522211031

ISBN 9987 - 438-07-5

## **Maelezo ya mwenezi**

Mnamo mwezi wa Novemba 1902, huko India mjadala ulifanyika baina ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala wa dhehebu la Ahli Hadithi na Sheikh Abdullah wa Chakrala wa dhehebu la Ahli Kurani. Sheikh wa kwanza alipandisha daraja la Hadithi kupita kiasi na Sheikh wa pili alikataa kabisa Hadithi, sawa na itikadi yao.

Seyyidna Ahmad a.s., tarehe 27 Novemba 1902, akaeleza kwa sura ya kijitabu maoni yake juu ya mjadala huo na akatoa nasaha kwa Jumuiya yake kuhusu habari hiyo :

"Waislamu wanavyo mkononi mwao vitu vitatu kwa kuimarika juu ya miongozo ya Kiislamu:

1. Kurani Tukufu ambacho ni Kitabu cha Mungu.....
2. Suna, ....kwa Suna tunamaanisha maelezo ya Mtume s.a.w. yaliyofululiza, yaliyokuwepo pamoja na Kurani Tukufu.
3. Hadithi, ...kwa Hadithi tunamaanisha athari zile za Mtume s.a.w. zilizokusanywa kwa njia ya wasimulizi mbali mbali kwa sura ya visa miaka mia na hamsini takriban baada ya Mtume s.a.w. Kwa hiyo kipambanuzi kati ya Suna na Hadithi ni kwamba Suna ni njia inayofululiza ya kutenda matendo aliyoianzisha Mtume s.a.w mwenyewe, nayo ni katika daraja la pili baada ya Kurani Tukufu katika madaraja ya yakini...Lakini Hadithi, Mtume s.a.w mwenyewe hakuziandikisha wala hakufanya mpango wowote wa

kuzikusanya."

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya wa Tanzania amefasiri kitabu hicho cha Seyyidna Ahmad a.s. kwa Kiswahili. Tafsiri hii ya Kiswahili ilisomwa kwa makini na wanalugha, bwana Mahmudu Hamsini Mubiru na Bi Razia Kaluta, ambao wakatoa baadhi ya mashauri mema.

Katika makao makuu Sheikh Jamil R. Rafiq na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, wabashiri wa zamani wa Kenya na Tanzania, wakiwa pamoja walichunguza kwa uangalifu sana tafsiri hii kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu.

Katika kukamilisha kazi hii, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal, Sheikh Mubarak Mahmood na Sharifu Tanvir Mujtaba pia wakasaidia kwa njia mbalimbali. Tafsiri hii ni tunda la '*Deski ya Kiswahili*.'

Wote walioshughulikia katika kazi hii kubwa wanastahili kuombewa. Mwenyezi Mungu awajaalie malipo bora na akubali juhudhi na huduma yao. Amin.

Ch. Muhammad Ali,  
Wakilut Tasnif,  
Tahrike Jadid,  
Rabwah Pakistan,  
23 Machi, 2008.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ  
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ<sup>١</sup>

MAONI YA MASIHI MAUD, MWAMUZI  
ALIYEFANYWA NA MUNGU, JUU YA MJADALA  
BAINA YA SHEIKH ABU SAID WA BATALA  
NA SHEIKH ABDULLAH WA CHAKRALA  
NA NASAHA KWA JUMUIYA YANGU.

Kutokana na maandishi ya makundi mawili, inaonekana sababu ya mjadala juu ya mada hii ni kuwa Sheikh Abdullah amechukulia Hadithi za Mtume s.a.w. kuwa kitu kisichofaa, na anatamka maneno ambayo hata kuyataja ni utovu wa adabu. Sheikh Muhammad Husain alitoa hoja dhidi yake kuwa endapo kweli Hadithi ni kitu kisichofaa, kisicho na maana, na hazitegemewi, hapo sehemu nyingi za ibada na mas'ala za fik'hi zitabatilika. Maana, maelezo ya maagizo ya Kurani Tukufu yanafahamika kupitia Hadithi; waila Kurani ikichukuliwa kuwa inatosha, kuna dalili gani kutokana na Kurani peke yake kwamba sala ya Alfajiri ina rakaa mbili za faradhi, magharibi rakaa tatu na sala tatu zilizobakia zina rakaa nne kila moja? Hoja hii ina nguvu sana ingawa ina kosa moja ndani yake, ndiyo maana Sheikh Abdullah hakutoa jibu la kuridhisha; katoa maneno ya upuuzi tu yasiyofaa hata kuandikwa. Naam, hatimaye matokeo ya hoja hii yakawa kwamba ikambidii Sheikh Abdullah abuni sala mpya ambayo

---

<sup>1</sup> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

Twamsifu Mungu na kumsalia Mtume Mtukufu.

haimo asilani katika madhehebu yote ya Kiislamu. Yeye ameondolea mbali *Attahiyatu*, sala ya Mtume na dua nyingine zote za Hadithi zinazoombwa katika sala; na mahali pake kaweka aya tu za Kurani. Kadhalika akageuza sana sala, jambo lisilo na haja lilezwe hapa. Na huenda atakuwa amefanya mabadiliko pia ndani ya mas'ala za Hija, Zaka na kadhalika. Lakini, je, ni kweli kuwa Hadithi ni kitu kisichofaa na kisicho na maana anavyodhani Sheikh Abdullah? La hasha! Mungu Apishe mbali.

Uhakika ni huu kuwa kundi moja kati ya mawili limeshika njia ya kuzidisha kupita kiasi, na la pili, njia ya kupunguza kupita kiasi. Kundi la kwanza, yaani la Sheikh Muhammad Husain, lina ukweli ndani ya jambo hili kuwa Hadithi za Mtume s.a.w zilizo *mar'fua, muttasila*<sup>2</sup> haziwezi kuhesabiwa kuwa ni kitu kisichofaa na kisicho na maana. Lakini asipojali kanuni ya kuhifadhi heshima ya kitu, anazidisha sana daraja la Hadithi kiasi cha kuivunjia heshima Kurani Tukufu na inalazimika kukataliwa. Wala hajali kupinga na kukinza Kurani Tukufu. Na anatanguliza kisa cha Hadithi juu ya visa vivilvyoelezewa bayana katika Kitabu cha Mungu. Na anatanguliza kwa kila hali maelezo ya Hadithi juu ya maelezo ya neno la Mungu. Hili ni kosa kubwa lililo wazi na ni kwenda kombo katika njia ya uadilifu. Mungu

---

<sup>2</sup> **Mar'fua:** Zile Hadithi ambazo katika Sanad zake msimulizi anasema kwamba yeye alipata kumsikia Mtume s.a.w. akisema kadha. Yaani sanad ya Hadithi imerufaishwa hadi kwa Mtume s.a.w.

**Muttasila:** Muttasila maana yake zilizounganika. Ni zile Hadithi ambazo Sanad zake zimeunganika wala hazikukatika po pote katika mnyororo mzima. Yaani katika mfululizo wa majina ya wasimulizi hakuna hata jina moja ambalo liliachwa kutajwa.

Mwenye Jalali Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

فِيَّ أَيِّ حَدِيثٍ بَعْدَ اللَّهِ وَآيَتِهِ يُؤْمِنُونَ<sup>3</sup> (٧)

Yaani, ni Hadithi gani watakayoamini baada ya Mungu na aya Zake. Hapa neno Hadithi ni nomino ya kwaida inayomaanisha 'Hadithi zote', ambayo inaeleza wazi wazi kuwa Hadithi yoyote iliyio kinyume na Kurani na inapingana nayo wala hakuna njia ya kuilinganisha itupilieni mbali. Na katika Hadithi hii pia kuna utabiri mmoja ambao kiishara unafahamika kutoka katika aya hii, nao ni huu ya kwamba Mwenyezi Mungu katika aya hii Anaashiria kwenye habari hii ya kuwa zama zitakuja juu ya umati huu ambapo baadhi ya watu wa umati huu wakiacha Kurani Tukufu watatenda sawa na Hadithi ambazo madhumuni yake yanapingana na kukinzana na madhumuni ya Kurani Tukufu. Ilmuradi dhehebu hili la *Ahli Hadithi* linakanyaga njia ya kuzidisha kupita kiasi kuhusu habari hii ya kwamba wanatanguliza maneno ya Hadithi juu ya ushahidi wa Kurani. Kama wangekuwa na uadilifu na ucha-Mungu wangeweza kulinganisha Hadithi kama hizo na Kurani Tukufu. Basi wakaridhika kuifanya kauli hasa ya Mungu kuwa kama kitu kilichoachwa, na wala hawakuridhika kwamba waziache Hadithi zote zinazopinzana na maneno ya Kitabu cha Mungu au wazilinganishe na Kitabu cha Mungu. Hii ndiyo njia ya kuzidisha sana aliyoifuata Sheikh Muhammad Husain.

Na mpinzani wake, Sheikh Abdullah, amechukua njia ya kupunguza kupita kiasi kwamba alizikataa Hadithi kabisa.

<sup>3</sup> Al-Jathia, 45:7

Na kuzikataa Hadithi kwa maana nyingine ni kuikataa Kurani Tukufu pia kwani Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Kurani Tukufu

فَلْ إِنْ كُنْتُمْ تَخْبُونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي مَحِبْبُكُمُ اللَّهُ<sup>4</sup>

Hivyo basi, kama kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu kunategemea kumfuata Mtume s.a.w. na ili kujua mifano ya matendo yake ambayo kumfuata yeye kunaitegemea, Hadithi pia ni njia mojawapo. Basi yule anayeacha Hadithi, huacha pia njia ya kumfuata. Na kauli ya Sheikh Abdullah kuwa Hadithi zote ni mkusanyiko wa shaka na dhana tu, ni wazo linalozalika kwa sababu ya upungufu wa fikara. Na chanzo cha wazo hilo ni mgawanyiko ulio na kosa na usiokamilika, ambao uliwapoteza watu wengi sana, kwani wakigawa wanasema kuwa mkononi mwetu mna Kitabu cha Mungu na Hadithi; Hadithi ndiyo kadhi kwa Kitabu cha Mungu, kana kwamba Hadithi zimejikalia kitu cha kadhi au jaji na Kurani Tukufu imesimama mbele yake kama mdai nayo iko chini ya amri ya Hadithi. Bila shaka kila mmoja atadanganyika kwa maneno haya ya kwamba Hadithi zimekusanywa miaka mia au mia na hamsini baada ya Mtume s.a.w. Na haziko salama kutiliwa mikono ya watu, na juu ya hayo ni rundo la *Ahaad*<sup>5</sup> si ya yakini. Na zile za aina ya *Mutawatirat*<sup>6</sup> ni chache na kwa nadra kana kwamba hazipo, tena hizo ndizo zilizo kadhi kwa Kurani Tukufu. Kwa hiyo italazimu kwamba dini nzima

<sup>4</sup> Sema ikiwa nyinyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni. (Aali-Imran, 3:32)

<sup>5</sup> Ahaad ni Hadithi zilizosimuliwa na mnyororo mmoja tu wa wasimulizi.

<sup>6</sup> Mutawatirati ni Hadithi ambazo muradi wake ni wazi sana na wasimulizi wake ni wengi mno hadi akili haiwezi kuwakadhibusiha.

ya Islam ni rundo la mambo ya dhana tu. Na ni dhahiri kuwa dhana si kitu chochote. Yule mtu anayefuata dhana tu amekuwa ameanguka chini sana kutoka kwenye mahali pa juu pa yakini ya kweli. Na Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّ الظُّلْمَ لَا يُعْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا<sup>7</sup>

Yaani dhana tupu si kitu chochote mbele ya yakini ya kweli. Hivyo basi, Kurani Tukufu ikaponyoka mkononi kwani bila fatuwa za kadhi si wajibu kutenda sawa nayo na ni kitu kilichotupwa na kuachwa. Na 'Kadhi', yaani Hadithi, 'amejivalia' mavazi machafu ya dhana tupu ambayo kwayo uwezekano wa uwongo hauondolewi. Kwani kifafanusi cha dhana ni hiki tu kwamba hiyo haiwi pasipo uwezekano wa uwongo. Katika hali hii Kurani haikubaki mkononi na Hadithi haifai kutegemewa. Ndiyo kusema kwamba zote mbili tumezikosa. Hilo ni kosa lililowaangamiza wengi.<sup>8</sup>

Na njia iliyonyoka ambayo kwa kuidhihirisha

<sup>7</sup> Yunus, 10:37

<sup>8</sup> Tanbihi: Nilipokwisha maliza kuandika tangazo hili (maoni haya), pengine mistari miwili mitatu ilibaki, ndipo nikazidiwa na usingizi hata kwamba nikalazimika kuacha karatasi na kulala. Nikawaona katika ruya Sheikh Muhammad Husain wa Batala na Shekh Abdullah wa Chakrala. Na nikawaambia kwa Kiarabu: حَسْفَ الْقَمَرِ وَالشَّفَنْ فِي رَمَضَانَ - فَبِأَيِّ الْآرْبَكُمَا تُنَذَّبِينَ vimekwisha patwa katika Ramadhani. Enyi mabwana wawili, kwa nini mnakadhibisha neema ya Mungu. Kisha namwambia ndugu Maulawii Abdul Karim katika ruya kwamba hapa neema muradi wake ndimi mimi. Kisha nikainua macho na kuangalia kwamba kuna ukumbi mmoja amabmo taa inawaka, yaani ndio wakati wa usiku na watu wachache wakifunua Kurani Tukufu mbele ya taa wanankuu mafungu hayo mawili ya ufunuo uliotajwa juu, kana kwamba huo umo ndani ya Kurani Tukufu kwa mpango huo. Nami nikamtambua mtu mmojawapo kwamba ndiye Bwana Mian Nabi Bakhsh wa Amritsar, mshonaji wa kutililia. *Mwandishi*

nimeandika makala haya ndiyo kwamba Waislamu wanavyo mkononi mwao vitu vitatu kwa kuimarika juu ya miongozo ya Kiislamu:

- (1) Kurani Tukufu iliyio Kitabu cha Mungu, ambayo hakuna maneno yoyote yawayo ya kweli kabisa na ya yakini zaidi kuliko hiyo, ni neno la Mungu. Hamna shaka wala dhana ndani yake.
- (2) Cha pili ni Suna. Hapa tunazungumzia bila kujali istilahi za Ahli Hadithi, yaani sisi hatuchukulii Suna na Hadithi kuwa kitu kimoja kama ilivyo dasturi ya Muhadithina (wataalamu wa Hadithi) wa kawaida; bali Hadithi ni kitu kimoja na Suna kitu kingine. Kwa Suna tunamaanisha mazoea ya matendo ya Mtume s.a.w yanayofululiza, yaliyokuwepo pamoja na Kurani Tukufu tangu mwanzo na yatadumu kuwa pamoja. Au kwa maneno mengine twaweza kusema kwamba Kurani Tukufu ni kauli ya Mwenyezi Mungu na Suna matendo ya Mtume wa Mungu s.a.w. Ni kawaida ya Mungu tangu kale kuwa manabii huleta kauli ya Mungu kwa kuwaongoza watu, nao hufafanua kauli hiyo kwa matendo yao ili watu wasiwe na shaka kufahamu kauli hiyo; wenyewe hutenda sawa na kauli hiyo na huitendesha kwa wengine pia.
- (3) Njia ya tatu ya mwongozo ni Hadithi. Na kwa Hadithi tunamaanisha simulizi zile zilizokusanywa kwa njia ya wasimulizi mbali mbali kwa sura ya visa miaka mia na hamsini takriban baada ya Mtume s.a.w. Kwa hiyo kipambanuzi kati ya Suna na Hadithi ni kwamba Suna ni njia inayofululiza ya kutenda matendo aliyoianzisha Mtume s.a.w mwenyewe, nayo ni katika daraja la pili baada ya Kurani

Tukufu katika madaraja ya yakini. Na kama Mtume s.a.w. alivyoagizwa kuieneza Kurani Tukufu, ndivyo alivyoagizwa pia kusimamia Suna. Hivyo basi, kama vile Kurani Tukufu ni ya yakini kabisa, ndivyo ilivyo ya yakini Suna ya amali inayofululiza. Huduma hizo zote mbili Mtume s.a.w. akazitekeleza kwa mkono wake mwenyewe na akajua hizo zote mbili ni faradhi yake. Kwa mfano agizo la kusali lilipotolewa, Mtume s.a.w. akaifafanua kauli hii ya Mwenyezi Mungu kwa tendo lake na kwa vitendo akadhihirisha kuwa raka za alfajiri ni hizi, na za magharibi hizi na kwa sala zilizobakia ni raka hizi na hizi. Kadhalika akaonyesha Hija kwa kuhiji; na mwenyewe kwa kuwafanya maelfu ya masahaba wafuate amali hiyo akaimarisha kabisa njia ya kutenda hivyo kufululiza. Basi mfano wa kitendo unaoshuhudiwa kwa vitendo na kujulika mpaka leo ndani ya umati wa Mtume s.a.w huitwa Suna. Lakini Hadithi, Mtume s.a.w mwenyewe hakuziandikisha wala hakufanya mpango wowote wa kuzikusanya.

Hadithi kadha alizikusanya Hadhrat Abu Bakr r.a, lakini kwa sababu ya ucha-Mungu akazichoma moto Hadithi zote akifikiria kuwa hakuzisikia hizo moja kwa moja kutoka kwa Mtume Mtukufu s.a.w., Mungu anajua uhakika ulivyo. Zama za Masahaba zilipokwishapita, ndipo baadhi ya Taba‘ Tabi‘<sup>9</sup> wakaelekezwa na Mungu kuwa Hadithi pia zapaswa kusanywa, ndipo Hadithi zikaanza kukusanywa. Hakuna shaka kuwa wengi wa waliozikusanya Hadithi walikuwa

---

<sup>9</sup> Waislamu waliowahi kuwaona Masahaba huitwa Tabi‘ina, na Waislamu waliowaona Tabi‘ina huitwa Taba‘ Tabi‘ina.

wacha-Mungu na watawa sana. Kadri walivyojaaliwa wakachambua Hadithi; na Hadithi zile walizoziona ni mionganini mwa zilizozushwa walijipusha nazo; na Hadithi ya kila msimulizi asiyejulikana maisha yake wazi hawakukubali. Wakajibidiisha sana, lakini kwa kuwa hayo yote yakafanyika baada ya wakati wake, hivyo kazi hii yote ikabaki katika daraja la dhana tu. Hata hivyo itakuwa kinyume cha uadilifu ikitsemwa kwamba Hadithi zote hizo ni upuuzi, bure, pasipo faida, na uzushi; bali kwa kuandika Hadithi hizo ukafanywa uangalifu, utafiti na uchambuzi kiasi hiki hata kwamba mfano wake hauonekani katika dini nyiginezo. Mayahudi wana Hadithi zao; na waliompinga Hadhrat Masihi a.s. walikuwa ni kundi lile la Mayahudi lililoitwa watendao sawa na Hadithi. Lakini haikuthibitishwa kuwa wataalamu wa Kiyahudi wa Hadithi walikusanya Hadithi zile kwa uangalifu kama walivyofanya wataalamu wa Kiislamu wa Hadithi. Hata hivyo ni kosa kudhania kuwa kabla Hadithi zilikuwa hazijakusanya watu walikuwa hawana habari za rakaa za sala au hawakujua taratibu za kuhiji. Kwani mfululizo wa matendo uliopatikana kwa njia ya Suna ulikuwa umewafundisha mipaka na faradhi zote za Kiislamu. Hivyo, basi, ni sawa kabisa kuwa hata kama Hadithi hizo zilizokusanya baada ya muda mrefu zisingekuwepo duniani mafundisho sahihi ya Islam yasingepata kasoro yoyote, kwani kwa vile Kurani Tukufu na mfululizo wa mfuatano wa matendo ukatosheleza mahitaji hayo. Hata hivyo Hadithi zikaongeza nuru hii, kana kwamba Islam ikawa nuru juu ya nuru. Hadithi zikasimama kama mashahidi wa Kurani na Suna. Na mionogi mwa madhehebu mengi ya Islam

yaliyozalika baadaye, dhehebu la kweli lilifaidika sana na Hadithi zilizo sahihi. Basi njia ya usalama zaidi ni hii tu kwamba tusiwe na imani kama Ahli Hadithi wa zama hizi kuhusu Hadithi kwamba hizo zaitangulia Kurani; na kama visa vya Hadithi vikipedia na maelezo ya Kurani hapo tusivikubali visa vya Hadithi na kuacha Kurani. Na wala zisichukuliwe Hadithi kitu kisicho na maana na batili kama ilivyo itikadi ya Sheikh Abdullah wa Chakrala. Bali yapasa Kurani na Suna zichukuliwe kuwa Kadhi juu ya Hadithi. Na Hadithi isiyo kinyume na Kurani na Suna ikubaliwe kwa moyo mkunjufu, na hii ndiyo njia iliyonyoka. Wamebarikiwa wale ambao wanafuata kanuni hii; ni mwenye bahati mbaya sana<sup>10</sup> na mpumbavu yule mtu ambaye bila kujali kanuni hii anazikataa Hadithi.

Jumuiya yetu yapaswa kuwajibikiwa kuwa kama

<sup>10</sup> Leo usiku nilioteshewa katika ruya kwamba kuna mti mmoja wenye matunda, ulio mzuri na wa kupendeza sana, na uliozaa kochokocho. Na watu kadha kwa kujikalifisha na kwa nguvu wanataka kupandisha juu yake mmea utambao usio na mzizi bali wamekwisha upandisha tayari. Mmea huo ni kama kimelea. Na kadiri mmea huo unavyopanda juu zaidi mtini unayaharibu matunda; na mti huo mzuri ukaanza kuwa na sura mbaya na ya kuchukiza na iko hatari kubwa ya kuharibika matunda yanayotazamiwa kutoekana na mti huu, bali kiasi fulani yamekwisha haribika tayari. Ndipo moyo wangu kwa kuona hali hiyo, ukahangaika na kuyeyuka. Nami nikamwuliza mtu mmoja mwema na mtukufu aliyekuwa amesimama, ni nini mti huu, na nini mmea huu ambao umeubana vikali mti huu mzuri? Akanijibu akisema kuwa mti huu ni Kurani Tukufu, Neno la Mungu; na mmea huu ni zile Hadithi na kauli na kadhalika zilizo kinyume na Kurani au zinazohesabiwa kuwa kiyume, na wingi wa hizo umeubana mti huu, nazo zinaendelea kuudhuru sana mti huu. Ndipo nikazinduka. Nikiamka tu wakati huu wa usiku ninaandika madhumuni haya na sasa namaliza; na huu ni usiku wa kuamkia Jumamosi na baada ya saa sita, ni saa nane kasoro dakika ishirini. **فَالْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى ذٰلِكَ** Basi Alhamdu lillahi kwa sababu hii. **M.G.A.**

Hadithi fulani haipingani wala haikinzani na Kurani na Suna, hata kama ni ya daraja la chini, waitekeleze na kuitanguliza juu ya fik'hi iliyoundwa na mtu. Na kama mas'ala fulani hazipatikani katika Hadithi wala katika Suna, na wala hazionekani katika Kurani, hapo wafuate fik'hi ya Kihanafii; kwani wingi wa wafiasi wa dhehebu hili ni dalili ya utashi wa Mungu. Na kwa sababu ya baadhi ya mabadiliko ya siku hizi, fik'hi ya Kihanafii isiweze kutoa fatuwa sahihi, hapo maulamaa wa silsila hii wafanye *ijtihadi* waliyojaaliwa na Mungu. Lakini wawe macho kwamba wasizikatae Hadithi bila sababu yoyote kama Sheikh Abdullah wa Chakrala. Naam, pale waonapo Hadithi inapingana na Kurani Tukufu na Suna, basi waiache Hadithi. Kumbukeni kuwa Jumuiya yetu iko karibu zaidi na Ahli Hadithi kuliko Abdullah. Mawazo ya kipuuzi ya Abdullah wa Chakrala hatuhusiani nayo kabisa. Yeyote aliyemo ndani ya Jumuiya yetu anapaswa azichukie kwa moyo na kukirihika itikadi za Abdullah wa Chakrala kuhusu Hadithi. Na wanafiri kabisa kukaa na watu wa aina hii kwani hilo ni dhehebu lililonagamia zaidi kuliko wapinzani wengine.<sup>11</sup> Na yapaswa wasielekee kukuza hadhi ya Hadithi kupita kiasi kama kundi la Sheikh Muhammad Husain, wala kuelekea kupunguza

---

<sup>11</sup> Usiku huu huu saa tisa na dakika mbili nimepata ufunuo kwa Kiarabu, nao ndio huu:

مَنْ أَغْرَضَ عَنْ ذِكْرِي نَبْتَلِيهِ بِذُرْرَةٍ فَاسِقَةٌ  
مُلْحَدَةٌ يَمْلِئُونَ إِلَى الدُّنْيَا وَ لَا يَعْبُدُونَنِي شَيْئًا

Yeyote atakayejitenga na Kurani tutamjaribia na wazao waovu watakaoishi wakimkana Mungu, wataiangukia dunia na hawatakuwa na sehemu yoyote katika ibada yangu; yaani huu ndio utakuwa mwisho wa wazao hawa, hawatajaaliwa toba wala ucha-Mungu. *Mwandishi*.

hadhi ya Hadithi kupita kiasi kama Abdullah. Bali watambue kuhusu habari hii kwamba njia ya wastani ndiyo njia yao; yaani, wasizichukulie sana Hadithi kuwa makusudio yao hasa hata kwamba Kurani ikabaki kama kitu kilichoachwa, na wala wasiziache Hadithi na kuzipuuza hata kwamba Hadithi ya Mtume s.a.w. zikapotea kabisa. Kadhalika yawapasa kwamba wasimkatae Mtume s.a.w kuwa *Khatamun Nabiyina* wala wasichukue muradi wake ule usababishao kufunga mlango wa kuongea na kuzungumza na Mwenyezi Mungu kwa umati huu. Na ikumbukwe kwamba imani yetu ni hii kuwa Kitabu cha mwisho na Sheria ya mwisho ni Kurani na baada yake mpaka siku ya Kiyama hakuna nabii atakayeleta Sheria au anayeweza kufunuliwa moja kwa moja bila kumfuata Mtume s.a.w., bali mlango umefungwa mpaka siku ya Kiyama. Na kwa kumfuata Mtume s.a.w milango iko wazi ya kupata neema ya wahyi mpaka siku ya Kiyama. Wahyi ulio natija ya ufuasi wa Mtume s.a.w. hautakatika kamwe, lakini unabii wenyе Sheria au wa kujitegemea umeisha koma.

وَلَا سَبِيلَ إِلَيْهَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَمَنْ قَاتَ  
إِنِّي لَسْتُ مِنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَ  
سَلَّمَ وَأَدْعُكُ أَنَّهُ نَبِيٌّ صَاحِبُ الشَّرِيعَةِ أَوْ مَنْ  
ذُوْنَ الشَّرِيعَةِ وَلَيْسَ مِنَ الْأُمَّةِ فَمَثُلُهُ كَمَثْلِ  
رُجُلٍ غَمَرَهُ السَّيِّئَاتُ الْمُنْهَمُرُ فَالْفَاهُ وَزَاهِهُ وَلَمْ  
يُغَادِرْ حَتَّى مَاتَ

Hakuna njia ya kuelekea kupata unabii huo hadi siku ya Kiyama. Na yule asemaye mimi simo katika umati wa Muhammad s.a.w. na akadai yu nabii mwenye sheria au bila

sheria lakini si katika umati wa Muhammad s.a.w. hali yake ni kama hali ya mtu aliyefunikwa na mafuriko ya maji yapitayo kwa kasi na kumtupa mbele yake na hayakumwacha hata kafa. Maelezo yake ni haya kuwa mahali ambapo Mwenyezi Mungu ameahidi kwamba Mtume s.a.w. ni Khatamul Ambiyaa, papo hapo aka-ashiria pia kuwa Mtume s.a.w. kwa nguvu zake za kiroho ni kama baba kwa watu wema ambao kwa sababu ya ufuasi wa Mtume s.a.w. nafsi zao hukamilishwa, hujaaliwa wahyi na heshima ya maongezi na Mungu, kama Yeye Mwenye jalali Asemavyo ndani ya Kurani Tukufu:

مَاكَانٌ مُّحَمَّدٌ أَبَابَاً أَحَدٍ مِّنْ رَّجَالِكُمْ  
وَلِكِنْ رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّنَ<sup>١٢</sup>

Yaani Mtume Muhammad s.a.w. si baba wa yejote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mungu na Khatamun Nabiyyin. Sasa ni dhahiri kwamba neno *lakin* katika lugha ya Kiarabu linatumika kwa ajili ya *Istidraki* yaani kuwahi kushika kilichoponyoka. Basi katika sehemu ya aya hii jambo lililohesabiwa limeponyoka yaani lililokanwa kupatikana katika dhati ya Mtume s.a.w., ni kuwa kwake baba wa mwanamume yejote kwa njia ya kiwiliwili; basi kwa kutumia neno *lakin*, jambo lililokuwa limeponyoka limelipwa kwa kumwita Mtume s.a.w. kuwa *Khatamul Ambiyaa*, linalomaanisha kwamba baada yake imekatika kupatikana moja kwa moja neema ya unabii; bali sasa ataipata yule tu ambaye atakuwa na muhuri wa ufuasi wa

---

<sup>12</sup>Al-Ahzab, 33:41

Mtume s.a.w juu ya amali zake, na kwa njia hii yeye atakuwa mwanaye Mtume s.a.w. na mrithi wake. Ilimuradi, kwa njia moja ubaba wa Mtume s.a.w. umekataliwa na kwa njia nyingine ubaba wake umethibitishwa ili upinzani uondolewe uliotajwa katika aya<sup>13</sup> انَّ شَيْئَكَ هُوَ الْأَبْرَزُ Natija ya aya hii ni kwamba ingawaje unabii bila Sheria umekatika katika maana hii kwamba mtu yejote hawezi kupata moja kwa moja cheo cha unabii lakini haukukatika kwa njia hii kwamba unabii huo unapatikana na kubarikiwa kutoka katika taa ya unabii wa Muhammad s.a.w. Yaani mtu mkamilifu huyo kwa jiha moja atokane na umati wa Mtume s.a.w. na kwa jiha nyingine awe na sifa kamili za unabii ndani yake kwa sababu ya kujipatia nuru za Muhammad s.a.w. Na kama kwa njia hiyo pia ukamilifu wa watu wenye vipawa wa umati wa Mtume s.a.w. ukikanwa, hapo, Mungu apishe mbali, Mtume s.a.w. ataonekana mkiwa kwa jiha zote mbili; hana mwana wa kimwili wala hana mwana wa kiroho; na mpinzani anaonekana mkweli anayemwita Mtume s.a.w mkiwa.

Sasa jambo hili kwa vile limeisha amuliwa kuwa unabii wa kujitegemea baada ya Mtume s.a.w. unaopatikana moja kwa moja bila kumpitia Yeye s.a.w.<sup>14</sup> mlango wake

<sup>13</sup> Hakika adui yako atakuwa mkiwa. Al-Kauthar, 108:4

<sup>14</sup> Baadhi ya masheikh wenye elimu haba wakinipinga wanasema kwamba Mtume wetu s.a.w. alitupa bishara kuwa madajali thelathini watatokea ndani yenu, na kila mmoja mionganoni mwao atajidai kuwa nabii. Jibu lake ni hili kwamba enyi wapumbavu, wenye bahati mbaya, bahati yenu ni kufikiwa na madajali tu thelathini! Sehemu ya tano ya karne ya kumi na nne ni karibu kumalizika, mwezi wa ukhalifa umekwishatimiza vituo kumi na vinne vya ukamilifu wake, habari ambayo kwayo aya hii inaashiria: وَالْقَمَرَ قَدَرْنَةً مَنَازِلٍ [Na mwezi tumeupimia vituo]. Yasiin, 36:40

umefungwa mpaka kiyama, na maadamu mtu hana ndani yake uhakika wa kuwa katika umati wa Mtume s.a.w. wala hajinasibishi kwa utumwa wa Muhammad s.a.w., hawezi kutumwa kwa njia yoyote baada ya Mtume s.a.w. hapo kumteremsha Hadhrat Isa a.s. kutoka mbinguni na kumchukulia kuwa ni mtu wa umati huu na unabii wake umepatikana na kubarikiwa kutokana na unabii wa Mtume s.a.w., ni uzushi mkubwa namna gani na kujikalifisha. Kumhusu mtu aliyekwisha kuwa nabii hapo kabla, itakuwaje sawa kusema kwamba unabii wake umetokana na taa ya unabii wa Mtume s.a.w. Na kama unabii hautokani na taa ya unabii wa Muhammad s.a.w., basi katika maana gani yeye ataitwa kuwa mwana-umati? Ni wazi kuwa maana ya kuwa mwana-umati haiwezi kuwa sawa kwa mtu mpaka kila sifa yake aipate kwa kumpitia nabii anayemfuata. Na yule mtu ambaye mwenyewe binafsi ana sifa kubwa ya kuitwa nabii, atakuwaje mwana-umati wa Mtume s.a.w.? Bali atakuwa nabii wa kujitegemea ambaye hana nafasi ya kutokea baada ya Mtume s.a.w. Mkisema unabii wake wa zamani alioupata moja kwa moja utaondolewa na sasa atapewa upya unabii mpya kwa kumfuata Mtume s.a.w. kama ilivyomaanishwa na aya hiyo.

---

Dunia inakaribia kufikia mwisho, lakini madajali wenu hawaishi, huenda wakadumu nanyi mpaka kufa kwenu. Enyi wapumbavu! Dajali yule anayeitwa shetani yumo ndani yenu nyinyi wenywewe, ndiyo maana hamwutambui wakati, hamziangalii ishara za kimbunguni. Lakini niwasikitikieje, yule aliyedhihiri kama mimi katika karne ya kumi na nne baada ya Musa a.s., naye aliiwa dajali na Mayahudi waovu. *فَالْقُلُوبُ تَشَابَهُتْ اللَّهُمَّ ارْجُمْ* Miyo imefanana. Ee Mungu, uhurumie.

*Mwandishi.*

Hapo umatii huu unaoitwa umati bora una haki kuwa mtu mmojawapo kutoka mionganini mwao afikie daraja hili la kuyumkinika kwa baraka ya kumfuata Nabii s.a.w. Wala hakuna haja ya kumshusha Hadhrat Isa a.s. kutoka mbinguni, maana anayetokana na umati huu anaweza kupata sifa kamilifu za unabii kutokana na nuru ya Muhammad s.a.w. Hapo kumshusha yejote mwengine ni kumnyanganya mwenye haki, haki yake. Na ni nani mwenye kumzuia mwana-umati asifikasiwe na baraka za Muhammad s.a.w. ili mfano wa baraka za Muhammad s.a.w. usifichikane kwa yejote awaye. Kwani kumfanya nabii kuwa nabii kuna maana gani? Kwa mfano, mtu fulani anadai anaweza kutengeneza dhahabu, na akiweka mmea fulani juu ya dhahabu yenyewe anasema haya dhahabu tayari, je, yaweza kuthibitika kwa hiyo yu mjuzi wa kutengeneza dhahabu? Ukamilifu wa baraka za Mtume s.a.w. ulikuwa kwamba mwana-umati apatiwe daraja hilo kwa mazoea ya kumfuata yeje s.a.w.; waila kumchukulia nabii mmoja aliye nabii tangu zamani kuwa mwana-umati kisha kumfikiria kwamba daraja la unabii alilo nalo ni kwa sababu ya yeje kuwa mwana-umati wala hakulipata moja kwa moja, ni uwongo mkubwa ulioje usiofaa kabisa. Bali mambo haya mawili yanapingana, kwani uhakika wa unabii wa Hadhrat Masihi ni huu kuwa yeje aliupata moja kwa moja bila kumfuata Mtume s.a.w.; na kama Hadhrat Isa a.s. afanywe mwana-umati kama inavyoeleza Hadithi<sup>15</sup> اَمَا مُكْمِنُكُمْ مُنْكِمٌ itamaanisha kuwa kila sifa yake kamilifu inatokana na baraka

---

<sup>15</sup> Imam wenu kutoka mionganini mwenu. (*Sahihibukhari, Kitabul Ambiyaa*)

za unabii wa Muhammad s.a.w.; na sasa hivi tuliisha kisia kuwa sifa kamilifu ya unabii wake haitokani na baraka za taa za unabii wa Muhammad s.a.w.; na huku ndiko kukutanisha mambo mawili yanayopingana, jambo ambalo ni batili kabissa. Kama mkisema Hadhrat Isa a.s. ataitwa mwana-umati huu lakini hatapata baraka yoyote kutoka kwa unabii wa Muhammad s.a.w., hapo uhakika wa kuwa mwana-umati utakosekana katika nafsi yake. Maana, tumekwisha zungumza sasa hivi kuwa hakuna maana nyiningine ya kuwa mwana-umati isipokuwa kwamba yeye awe na sifa ya ufuasi wake tu kama ilivyofafanuliwa katika Kurani Tukufu katika sehemu nydingi. Kwa vile kwa ajili ya mwana-umati mlango huu uko wazi wa kupata baraka hizi kutoka kwa nabii anayemfuata, hapo kuchagua njia ya uzushi na kuhalalisha mambo mawili yanayopingana kukutanisha ni upumbavu mkubwa sana; ataitwaje mwana-umati yule asiyepata sifa yoyote kutokana na ufuasi. Hapa upinzani wa baadhi ya wajinga pia unaondolewa ya kwamba kwa madai ya kupata wahyi wa Mungu yalazimu kwamba wahyi huo uwe katika lugha ya mdai si kwa Kiarabu. Kwani yule tu hulazimika kupata wahyi katika lugha ya kwao anayedai unabii kwa kujitegemea pasipo kunufaika na taa ya unabii wa Muhammad s.a.w. Lakini mtu ambaye akiwa mwana-umati anajichukulia nuru ya unabii kutoka katika baraka za Muhammad s.a.w. huwa anapata wahyi wakati wa maongezi na Mungu katika lugha ya nabii wake anayemfuata ili iwe ni alama mojawapo baina ya mfuasi na mfuatwa ihakikishayo uhusiano kati yao. Ni masikitiko, watu hao wanamdhulumu Hadhrat Isa a.s. kwa kila njia. Kwanza, pasipo kuondolea

mbali upinzani kwamba alilaaniwa wanampaza mbinguni mwili wake, na hivyo bado wanadaiwa na Mayahudi majibu ya upinzani wao. Pili, wanasema kuwa ndani ya Kurani kifo chake hakikutajwa popote, kana kwamba wanaleta sababu ya Uungu wake. Tatu, katika hali yake ya kushindwa wanamsukuma kumpeleka mbinguni. Yule nabii ambaye hata wanafunzi wake kumi na wawili hawapo ardhini na kazi ya mahubiri haijakamilika, kumpandisha mbinguni ni kama kumtupa motoni. Maana, roho yake inataka kukamilisha mahubiri, lakini anakalishwa mbinguni kinyume cha ridhaa yake. Mimi najiona nafsi yangu kwamba bila kukamilisha kazi yangu kama niinuliwe mbinguni nikiwa hai na hata kama nifikishwe kwenye mbingu ya saba sitakuwa na furaha. Kwani kama kazi yangu ina kasoro, mimi nitakuwa na furaha gani? Kadhalika ye ye naye hana furaha ya kwenda mbinguni. Huo ulikuwa ni uhajiri wa kisirisiri ambao wapumbavu waliuchukulia ni kwenda mbinguni. Mungu awaongoze. ﷺ نَعَمْ مَنِ اتَّبَعَ الْهُدًى Na amani iwe kwa yule afuataye mwongozo.

Mtangazaji

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

27 Novemba, 1902.